

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

*Anwani ya Simu: "REGCOM"
Simu ya mdomo: (028) 2220215-18
E-mail: ras.kagera@pmoralg.go.tz
Fax: (028) 2222341 / 2221356*



**OFISI YA MKUU WA MKOA
S. L. P. 299,
BUKOBA - KAGERA.
TANZANIA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
TAREHE 03 NOVEMBA, 2017**

Ndugu Wananchi, Napenda kutoa taarifa ya ziara ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli Mkoani Kagera kuanzia tarehe 06 hadi 09 Novemba, 2017.

Ndugu Wananchi, Dhumuni la ziara ya Mhe. Rais Magufuli ni kuwatemelea wananchi wa Mkoa wa Kagera pia kutembelea na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo Mkoani hapa. Vilevile Mhe. Rais Magufuli atapata fursa ya kuongea nanyi kwenye Mkutano wa Hadhara Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Ndugu Wananchi, Mhe. Rais Magufuli atawasili Mkoani Kagera tarehe 06.11.2017 siku ya Jumatatu mchana na atapokelewa na viongozi mbalimbali wa Mkoa. Aidha Mhe. Rais Magufuli ataanza ziara yake siku hiyo ya tarehe 06.11.2017 katika Manispaa ya Bukoba kwa kuzindua Uwanja wa Ndege wa Bukoba saa 08:00 mchana. Aidha, mara baada ya uzinduzi Mhe. Rais ataongea na wananchi katika Mkutano wa Hadhara.

Tarehe 07.11.2017 siku ya Jumanne Mhe. Rais Magufuli ataaelekea Wilayani Karagwe katika eneo la Nyakahanga na kuzindua Barabara ya Kyaka Bugene majira ya 03:00 Asubuhi na mara baada ya uzinduzi huo Mhe. Rais atasalimia wananchi.

Ndugu Wananchi, Vilevile Mhe. Rais Magufuli ataendelea na ziara yake Mkoani hapa tarehe 8.11.2017 siku ya Jumatano kwa kutembelea kiwanda cha Kagera Sukari Wilayani Missenyi ambapo atapata fursa ya kukagua mashamba ya miwa pia na kuongea na Wafanyakazi, Uongozi na Menejimenti ya Kiwanda hicho.

Ndugu Wananchi, Mhe. Magufuli atahitimisha ziara yake Mkoani Kagera tarehe 9.11.2017 siku ya Alhamisi katika Wilaya ya Missenyi kwa kuzindua Kituo cha Pamoja cha Forodha katika eneo la Mtukula mpakani mwa Tanzania na Uganda akiwa na Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni. Baada ya uzinduzi Ma-Rais wote watasalimia wananchi.

Ndugu Wananchi, Wito wangu kwa wananchi wote wa Mkoa wa Kagera ni kujitokeza kwa wingi kumpokea na kumshangilia Mhe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sehemu zote atakazopita kuanzia Nyakabango Wilayani Muleba Mpakani mwa Mkoza wa Geita na Kagera pia na maeneo yote yaliyotajwa atakapokuwa anatembelea, anazindua miradi ya maendeleo na atakapokuwa anaongea nasi.

Ndugu Wananchi, Nasisitiza kuwa wananchi wote tudumishe utulivu, amani na mshikamano na upendo kama ilivyo kawaida na desturi ya Mkoza wetu wa Kagera wakati tunapotembelewa na wageni hasa ugeni mkubwa kama wa Mhe. Rais wetu.

Aidha, nawahakikisha wananchi kuwa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama viro imara na vinaendelea na kazi yake ya kudumisha amani na utulivu. Nitumie fursa hii kuwaasa wananchi wote kujiepusha na

vitendo vyote vya uvunjifu wa amani. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya yejote atakayethubutu kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani.

Ndugu Wananchi, Mwisho, natoa wito tena kwenu wote kujitokeza kwa wingi tumpokee Rais wetu mpendwa **Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli** Mkoani kwetu Kagera.

Kagera: Kazi Amani na Maendeleo.

Kazi Amani na Maendeleo: Kagera

Imetolewa na; Mhe. Meja Jenerali (Mst) Salum M. Kijuu

Mkuu wa Mkoa

KAGERA